

**Taarifa ya ziara ya Tanga kuhusu mradi wa barabara za halmashauri ya Tanga
22/12/2009**

Tarehe 22/12/2009 tulikutana na injinia wa mkoa wa Tanga pamoja na msaidizi wake injinia Mr Lema. RP. Msaidizi wake ni Mr Kaniki Arafat pamoja na Dominata Rwechungura na Hamadi Bwaja wa UWABA na Uli Malsius. Walitupokea vizuri na kusema walishapata taarifa za UWABA kutoka kwa UWP wakishauliana juu ya uwezekano wa kwepo barabara za wapanda baisikeli katika mradi unaendelea. Tulikubaliana kwa pamoja tuzitemblea barabara zote zilizopo kwenye mradi ili tuweze kutoa ushauri wetu.

Tarehe 23/12/2009 tulikutana na Meya wa Tanga. Tulifanya kikao kufupi tukiwa na Uli Malsius, Dominata Rwechungura, Hamadi Bwaja, Rashid, Idrisa, Mbayara. Tulikubaliana panapowezekana lazima pawepo barabara za wapanda baisikeli baada ya kikao na Meya tulienda kutembelea barabara zote zilizopo kwenye mradi baadaye ya kuziona ulishauliana barabara 6 ambazo ni

- 1) Karume Road 8 km iwepo barabara ya wapanda baisikeli
- 2) Makoko road 0.6 km barabara ya wapanda baisikeli
- 3) No 08 Road mchoro wa wapanda baisikeli au vibao vinavyoonyesha sehemu yao kupita
- 4) Msambweni road 3.3 km barabara ya wapanda baisikeli
- 5) Duga airport road 4 km barabara ya wapanda baisikeli
- 6) Mnyanjani road 3km barabara ya wapanda baisikeli

Kuhusu barabara ya Pangani kutoingizwa kwenye mradi wakati yenyewe ndio yenye matumizi makubwa ya baisikeli na yenye ajali nyingi ya baisikeli na uchumi mkubwa kwa wapanda baisikeli unategemea barabara ya Pangani. Mradi ni wa barabara za Halmashauri wakati barabara ya Pangani ni barabara ya TANROADS. Hivyo ni kazi ya UWABA kushauri TANROADS makao makuu umuhimu wa barabara ya Pangani na matumizi ya wapanda baisikeli na ajali nyingi zinavyotokea kila wakati katika mipangango yao wanaweza kuipa kipaumbele barabara ya Pangani hata kuiombea pesa.

Ni muhimu kukutana haraka na ofisi ya UWP consulting ili kuwapa taarifa na makubaliano na mahitaji ya watu wa Tanga kuhusu barabara tulizokubaliana zijengwe barabara za wapanda baisikeli.

Mikoa ambayo imo kwenye mradi wa barabara za Halmashauri ni (7) – Tanga, Arusha, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Kigoma, Mwanza. Mikoa yote inatatizo la kutokuwepo miundombinu ya matengnezo ya barabara za wapanda baisikeli watembea kwa miguu na walemavu na mikoa yote matumizi ya baisikeli yanakua ka kasi kubwa.

Hata kama hawana elimu ya matumizi ya barabara na usalama wao ni vyema barabara za wapanda baisikeli zikajengwa ili wakipata elimu ya usalama na matumizi ya barabara tayari barabara zao zipo unawaelekeza pakwenda.

Vilevile mahitaji ya barabara za Halmashauri yanakuwa yamekamili kwa kuondoa msongamano wa magari ambao unaweza kujitokeza hapo badaye

Utaalamu ukitumika vizuri mahitaji yote yanaweza kukamilika tena kwa gharama nafuu

Changamoto kwa UWABA

Ni lazima kukutana na Consulting wa barabara za Mbeya, Mtwara, Kigoma, Mwanza kutoa ushauri wa kuwepo barabara za wapanda baisikeli kama tulivyofanya Tanga.

Ukimaliza kushauri consulting ni muhimu watu kwenda kukutan na Halmashuari za mikoa husika pamoja na injinia wa mkoa kushaurian pia na kutembelea zile barabara ambazo zipo kwenye mradi kazi hiyo inatakiwa kuanza haraka sana kwani mikoa husika imeshaanza hatua ya kwanza.